OFISI YA RAIS TAMISEMI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

SHULE YA SEKONDARI UHAMIAJI

S.L.P 45058

DAR-ES-SALAAM

Kumb Na. TMC/USS/JI/2O21/----------

JINA LA MWANAFUNZI ----------

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI UHAMIAJI.

1.0 **UTANGULIZI**

Mkuu wa shule ya sekondari UHAMIAJI anayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha ----------katika shule hii kwa mwaka wa masomo----------

KARIBU SANA.

Shule itafunguliwa tarehe---------- na mwisho wa kuripoti ni tarehe ----------(ndani ya siku 14).

2.0 **MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ipo jirani na ofisi ya uhamiaji makao makuu Kurasini. Umbali wa $^{1}/_{2}$ kilometa kutoka kituo cha JKT barabara ya Kilwa upande wa kulia ukitokea mbagala.

2.1 **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.2 **Sare za shule**

a) Wavulana

- Suruali mbili(2) za rangi ya bluu bahari zenye mkunjo wa nje chini(TURNUP). Rinda mbili za kiunoni kwa mbele(Celebration) na isiobana chini (Isiwe modal).
- Shati mbili(2) nyeupe tetron mikono mifupi isiyo na mitindo
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na soli fupi jozi mbili(2)
- Soksi nyeusi jozi mbili(2)
- Mkanda mweusi wa ngozi usio na urembo wala bakozi kubwa

b) Wasichana

- Sketi mbili(2) za rangi ya bluu bahari belt $2^{1}/_{2}$ rinda za kupanga ,wasiovaa hijabu urefu usipungue nchi tatu chini ya magoti na kwa wanaovaa hijabu urefu wa sketi uguse viatu
- Shati mbili(2) nyeupe tetroni, mikono mifupi kwa wasiovaa hijabu. Kwa wanaovaa hijabu juba liwe kubwa na linalovuka kitovu na nusu kanzu isiobana, aina ya kitambaa iwe haluwa

- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye mkanda mmoja kwa juu na soli fupi jozi(2)
- Soksi nyeupe ndefu(stoking) jozi mbili(2).

3.1 MAHITAJI MENGINE

c) Nywele

- Nywele ziwe fupi zinazochanwa na kitana kidogo na zisinyolewe kwa mitindo ya kihuni.
- Begi imara la mgongoni la kubebea madaftari na vitabu.
- Daftari kumi kaunta buku, kalamu, mkebe wa hisabati, kamusi ya Kiswahili kwa Kiswahili na kamusi ya kiingereza kwa kiingereza.

d) Sare za michezo

- Bukta ya daki bluu, Tishirt ya daki bluu pamoja na raba nyeusi kwa wavulana.
- Tishirt ya daki bluu, skin tight ndefu na raba nyeupe kwa wasichana.

3.2 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elemu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana na Elimu nchini na Ofisi ya Rais –TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo, yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

c) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazo pangiwa.

d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako.

e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi, na mazingira ya shule.

f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na.

h) Kutunza mali za umma.

3.3 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWA SHULE.

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Kucheza kamari
e) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile Uvutaji bangi , cocaine, Mirungi, Kuberi, n.k.
f) Kupiga au kupigana.
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba/ kusababisha mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongeza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi
n) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
o) Kumnyanyasa mwanafunzi kwa sababu ya ugeni, au jinsi yake, au umbile lake, au dini yake, au rangi yake.
p) Kumtukana matusi mwalimu, mfanyakazi au mwanafunzi mwenzako.
q) Utoro sugu kwa zaidi ya siku 90 mfululizo.

3.4 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI

a) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospital ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara mwanafunzi atakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maendeleo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

3.5 TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEKEZO/ MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

Karibu sana katika shule ya sekondari Uhamiaji.

…….

MKUU WA SHULE

FOMU YA KUKUBALI MASHARTI NA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI UHAMIAJI

A. IJAZWE NA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la mwanafunzi----------
2. Taifa ----------
3. Uraia----------
4. Dini----------
5. Tarehe ya kuzaliwa----------
6. Shule ya msingi uliosoma ----------
7. Mwaka uliomaliza shule ya msingi----------

Sahihi ya mwanafunzi----------

B. MAELEZO BINAFSI YA MZAZI/ MLEZI

1. Jina kamili la mzazi au mlezi----------
2. Anuani kamili ya mzazi/ mlezi----------
3. Mkoa----------Wilaya----------
4. Kata----------Mtaa----------
5. Namba ya nyumba ----------
6. Namba ya simu----------

Sahihi ya mzazi/mlezi----------

C. MAELEZO YA KIKAZI YA MZAZI/MLEZI

- Jina la mwajiri na idara----------
- Anuani yake----------
- Namba ya simu----------
- Kazi ya mzazi au mlezi----------

D. SOMO LA DINI

Mimi ----------ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi----------Kidato cha ---------- ninaruhusu mtoto wangu kuhudhuria somo la Dini ya ---------- dhehebu la ---------- siku ya jumatano akiwa shuleni Uhamiaji.

Sahihi ya mzazi/mlezi----------

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

STATION…….

DATE…….

PART A:

TO:

Medical officer

……..

……..

Miss/Mr…….

Please examine the above named as to his/her fitness for admission as a student in the following common diseases/problem.

Put a tick (v) for positive and a cross (x) for negative against in a box provided.

Pregnancy	
Asthma	
Sight	
Diabetes	
Worms (Stool)	
Epilepsy	
TB(Tuberculosis)	
Sickle Cell	
Heart Disease	
Yellow Fever	
U.T.I	
Hearing	

PART B: MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a medical officer)

I have examined the above named and consider that she/he is physically FIT/UNFIT for admission.

Date……Signature……

Station…… Designation……